**Wilaya ya Tunduru ilivyobarikiwa kuwa aina mbalimbali za madini ya vito**

**Na Albano Midelo**

WILAYA ya Tunduru iliyopo mkoani Ruvuma ina utajiri wa karibu aina zote za madini ya vito isipokuwa madini ya tanzanite ambayo katika dunia nzima yanapatikana Mirerani mkoani Manyara.



Kulingana na utafiti uliofanywa,madini yaliopo Tunduru ni safaya, Alexanderyte, Krizobery, almasi, dhahabu,pink safaya,blue safaya,topaz,wats,spinery, Changecoureganet, redganet,silicon,Rubi na madini mengineyo mengi.

Akizungumzia historia ya uchimbaji wa madini katika Wilaya ya Tunduru,Afisa Madini wa Wilaya ya Tunduru Mjiolojia Abraham Nkya anasema uchimbaji ulianza tangu mwaka 1995 na kwamba kutokana na uwepo wa madini mengi kipindi hicho watu wengi waliacha kazi serikalini na kujiingiza katika kazi hiyo.

Anasema kipindi hicho madini yalikuwa mengi na mchakato wa utengenezaji wa madini kijiolojia unachukua mamilioni ya mwaka na kila yanapochimbwa yanapungua na hatimaye yanawezakwisha

hivyo ameshauri kuwa makini kuhakikisha madini yanapochimbwa yanawanufaisha watanzania kabla ya hayajamalizika.



Hata hivyo anasema Idara ya Madini imesimamia ipasavyo wanunuzi wakubwa wa madini ya vito katika Wilaya ya Tunduru ambapo kwa mara ya kwanza katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 wamelipa ushuru wa huduma katika Halmashauri ya Tunduru kiasi cha shilingi milioni 66.

“Hatuwezi kuwalaumu wanunuzi wakubwa wa madini ya vito kwa kutolipa kodi mbalimbali serikalini tangu mwaka 1995,wanaostahili kulaumiwa ni watendaji waliokuwepo madarakani katika kipindi hicho kwa kuwa walishindwa kufanyakazi ya usimamizi wa madini hayo kwa mujibu wa sheria,usimamizi ulikuwa ni hafifu hali iliyoikosesha serikali mapato”,anasisitiza Nkya.

Anabainisha zaidi kuwa kipindi cha nyuma kabla ya serikali ya awamu ya tano,sekta ya madini ilishindwa kuwanufaisha watanzania ambapo Rais Dkt.John Magufuli baada ya kuingia madarakani amefanya mabadiliko makubwa katika sekta ya madini ikiwemo kubadilisha sheria ya madini na kuweka nidhamu katika sekta hiyo hali ambayo imesababisha watanzania kuanza kunufaika katika sekta hiyo.

Anasema yeye binafsi hawezi kuwalaumu wafanyabiashara wa madini ya vito moja kwa moja,kwa kuwa watendaji kipindi chote hicho tangu mwaka 1995 hadi 2015 walishindwa kusimamia ipasavyo sekta ya madini.

Anasisitiza kuwa katika mwaka 2016/2017 wanunuzi hao wa madini ya vito baada ya kusimamiwa ipasavyo na Idara ya madini kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru na TRA wamefanikiwa kukusanya kile ambacho kinapaswa kulipwa serikalini baada ya kupoteza mapato hayo kwa miaka mingi.

“Udhaifu wa kutosimamia sheria za madini toka kwa viongozi waliopewa mamlaka ambapo sheria inatamka wazi kuwa ushuru wa huduma unatakiwa kulipwa asilimia tatu ya mapato yaliokusanywa katika biashara husika kwa mwaka hivyo sheria inatakiwa kusimimamamiwa”,anasisitiza Mjiolojia Nkya.

Anasema ushuru wa huduma wa asilimia tatu unatakiwa kulipwa na wafanyabiashara wote wakiwemo wanunuzi wa madini na wachimbaji wadogo ambao wanakatwa asilimia tano ya mauzo ya madini toka kwa wanunuzi wa madini.

Afisa Madini huyo wa wilaya ya Tunduru anasisitiza kuwa hivi sasa malipo hayo yanalipwa vizuri Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya madini hali ambayo imesababisha sasa serikali kuanza kupata mapato halali.



Madini mengine yenye thamani kubwa aina ya shaba ya yamegundulika katika Kata ya Mbesa Tarafa ya Nalasi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.

Kugundulika kwa madini hayo kunaifanya wilaya ya Tunduru kuwa ndiyo wilaya pekee nchini na Afrika Mashariki na Kati kuwa na madini ya shaba mbalimbali zikiwemo kijani,bluu na njano.

Utafiti unaonesha kuwa Tarafa nzima ya Nalasi ina utajiri wa madini hayo ambayo yanaweza kuchangia kuinua uchumi wa wilaya hiyo,Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla wake.

Utafiti wa awali umebaini madini hayo yameenea hadi mto Ruvuma mpakani na nchi jirani ya Msumbiji na pia madini hayo yamesambaa hadi mpakani na wilaya ya Namtumbo.

Utafiti wa awali wa kijiolojia uliofanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1988 katika eneo la Kata ya Mbesa wilayani Tunduru umebaini kuwepo kwa mashapo ya madini ya shaba.

Utafiti huo wa awali ambao ulifanywa na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) umeonesha kuwepo kwa ubora wa mashapo ya shaba.

Afisa Madini wa Wilaya ya Tunduru Mjiolojia Abraham Nkya anasema ni kweli utafiti wa awali umebaini kuwepo kwa aina mbalimbali za madini ya shaba yakiwemo ya shaba ya bluu,njano na kijani.

Anasema serikali ilitenga eneo la Mbesa kwa ajili ya kuendelea kufanya utafiti wa madini hayo,hata hivyo changamoto iliyojitokeza ni kwamba serikali ilitenga eneo la Mbesa lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 1500 kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kwamba leseni zilitolewa zaidi ya 1000.

Hata hivyo anasema wachimbaji wadogo hao wameshindwa kuendeleza eneo hilo kwa sababu uchimbaji wa madini ya shaba ni tofauti ya uchimbaji wa madini ya vito.

“Madini ya shaba hauwezi kutumia sululu na chepe,bali madini ya shaba unatakiwa utumie baruti kuvunja mwamba,mitambo mikubwa na kuchakata miamba hiyo ili uweze kupata shaba yako kwa hiyo madini ya shaba yanahitaji uwe na mtaji mkubwa ‘’,anasisitiza Nkya.

Hata hivyo anasema madini ya shaba yanahitaji kufanya utafiti wa kina ili kugundua kiasi sahihi cha mashapo ya shaba yaliopo katika eneo husika kufahamu ubora wake  pia kutambua shaba hiyo itachimbwa kwa miaka mingapi.

Anabainisha kuwa hali hiyo ndiyo iliyosababisha hadi sasa wachimbaji wadogo waliopewa eneo la Mbesa kushindwa kuendeleza kwenye madini hayo na kwamba kati ya leseni zaidi ya 1000 zilizotolewa kwa wachimbaji wadogo ni wachimbaji wenye leseni mbili tu walijaribu kuanza kuendeleza miaka ya nyuma maeneo ya mgodi ambapo hivi sasa wote wameacha.

Anasisitiza kuwa kinachotakiwa hivi sasa ni kufanya utafiti wa kutosha kuhusiana na madini hayo na kwamba utafiti unahitaji rasilimali fedha na watu ambapo wachimbaji wadogo hawawezi kufanya utafiti kwa kuwa wao wanataka kuchimba madini na kuuza ili kupata fedha.

Ameongeza kuwa madini ya shaba yanauzwa kwa tani tofauti na madini ya vito ambayo yanauzwa kwa gramu ambapo Mchimbaji anaweza kuuza gramu moja na kupata fedha zake na kwamba hata uchimbaji wake ni rahisi sio sawa na madini ya shaba.

Hata hivyo anasema ubora wa shaba inayochimbwa Mbesa unafahamika ndiyo maana baadhi ya wachimbaji walianza kuchimba,kitu ambacho bado hakifahamiki ni kiasi cha madini yaliopo na muda wa kuchimbwa na kwamba kulingana na sheria ya madini iliyoboreshwa ya mwaka 2017, madini ghafi hayaruhusiwi kusafirishwa nje ya nchi.

Anabainisha kuwa inatakiwa mtambo wa kuyaongezea thamani madini ya shaba kufungwa katika eneo la Mbesa ili kuongeza thamani na kupata madini halisi ya shaba .

Kulingana na Afisa Madini,huyo leseni zilizotolewa kwa wachimbaji wadogo,leseni nyingi zimefutwa kwa sababu wameshindwa kuzilipia ada za mwaka na kushindwa kuziendeleza kwa sababu ya ukosefu wa mitaji na taarifa za kijiolojia,kijiofizikia na kijiokemia zimeshindwa kujua kiwango halisi cha shaba kilichopo Mbesa na ubora wake ili waweze kuchimba kwa faida ,kuchakata na kuuza.

Akizungumzia kuhusu malipo ambayo yanatakiwa kulipwa na Kampuni yoyote inayochukua madini ya ujenzi katika eneo lenye rasilimali,Afisa Madini huyo wa Wilaya ya Tunduru anasema,kampuni ya ujenzi inayochukua vifusi,mchanga na mawe inatakiwa kulipa katika ofisi ya madini mrabaha(Royality) ya asilimia tatu ya thamani ya yale madini kwa sababu yatakuwa katika mkataba wao(BOQ).




Anasema Kampuni hiyo pia inatakiwa kulipa ushuru wa huduma(Service levy) katika Halmashauri husika na kwamba Kata husika ambako madini hayo ya ujenzi yanatolewa inatakiwa kuchangia huduma za jamii ili kufidia uharibifu ambao unafanyika katika eneo husika.

“Kampuni inatakiwa kuwajibika kijamii kwa sababu madini hayo ya ujenzi yanachukuliwa katika jamii husika kwanini wasiwasaidie

kama wana mahitaji fulani ya kijamii kama choo,maji au zahanati hili lazima wawajibike",anasisitiza Nkya.

Hata hivyo anasema Halmashauri inapopata malipo ya ushuru wa huduma huwa inagawa asilimia 20 ya mapato yake kwa kila kijiji au mtaa lakini huwa haisemi kuwa malipo hayo imeyapata kwa Mkandarasi fulani.

Naibu Waziri wa Madini, Dotto Biteko 19 Julai, 2018 akizungumza na wanunuzi wa madini ya vito wilayani Tunduru alisema kuwa wanunuzi wa madini aina ya vito kote nchini wasiokuwa na mashine kwa ajili ya kukata na kung'arisha madini hayo watanyang'anywa leseni kwa kuwa wanaendesha biashara kinyume cha Sheria ya Mpya ya Madini ya Mwaka 2017.

"Sheria inamtaka mnunuzi ambaye ni mtanzania kuwa na mashine tano na mnunuzi wa kigeni kuwa na mashine 30 za kukata na kung'arisha madini ya vito, tunataka madini haya yaongezwe thamani ndani ya nchi ili kuongeza mapato serikalini," alisema Biteko.

Biteko alimuagiza Afisa Madini wa Tunduru Mjiolojia Abraham Nkya kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Juma Zuberi Homera na Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Wilaya kufanya ukaguzi kwenye maduka ya wanunuzi watakaopewa leseni mpya ili kubaini kama wana mashine za kukata na kung'arisha vito na kuchukua hatua za kisheria kwa wanunuzi watakaobainika kutokuwa na mashine hizo.

**Moja ya vipengere muhimu katika Sheria mpya ya madini ya mwaka 2017 iliyofanyiwa** marekebisho kutoka sheria ya madini ya mwaka 2010 ni pamoja na kuongezeka kwa malipo ya mrabaha kutoka asilimia nne hadi kufikia asilimia sita kwa madini ya metali yakiwemo dhahabu,shaba na fedha na kuongezeka kwa malipo ya mrabaha kutoka asilimia tano hadi sita kwa madini ya vito yakiwemo rubi,garnets na tanzanite.

Kupitia marekebisho ya sheria ya fedha na sheria ya kodi hivi sasa kila Kampuni au mtu anayetaka kusafirisha madini nje ya nchi,madini yatakaguliwa na kuthaminishwa na atalipa ada ya

ukaguzi ambayo ni asilimia moja ya thamani ya madini anayosafirisha.

Mchimbaji mdogo anayeuza madini kwa wanunuzi wa kati(Brokers) au wanunuzi wakubwa(Dealers) atakatwa asilimia tano ya thamani ya madini na kupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA).

**Mwandishi wa makala haya ni Mchangiaji wa gazeti hili,mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**